

**TAARIFA YA HALI YA WILAYA YA ILEMELA KWA MKUU WA MKOA WA MWANZA MHE. ADAM KIGOMA MALIMA KATIKA ZIARA YAKE WILAYANI
ILEMELA TAREHE 04/08/2022**

1. UTANGULIZI

1.1 KUANZISHWA KWA WILAYA

Wilaya ya Ilemela ilianzishwa rasmi mwaka 2002 na Rais wa Awamu ya Tatu kwa Mamlaka aliyopewa na Ibara ya 2 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 sambamba na Kifungu cha 6 cha Sheria Na.12 ya Mwaka 1994. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ikaanzishwa na kuanza utekelezaji wa shughuli zake katika bajeti ya kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013.

1.2 ENEO

Wilaya ya Ilemela ina ukubwa wa eneo lipatalo kilomita za mraba 1080.55. Kati ya hizo kilomita za mraba 828.45 (76.7%) zimefunkwa na maji na kilomita mraba 252.10 (23.3%) ni nchi kavu. Eneo la Wilaya ya Ilemela ni sawa na asilimia 3.1 ya eneo lote la Mkoa wa Mwanza ambalo ni kilomita za mraba 35,187 ambapo kati ya hizo kilomita za mraba 20,095 ni nchi kavu na kilomita za mraba 15,092 ni maji ya Ziwa Victoria.

1.3 MIPAKA

Wilaya ya Ilemela ipo upande wa Kusini mwa Ziwa Victoria. Magharibi imepakana na Ziwa Victoria, Mashariki imepakana na Wilaya ya Magu na Kusini Wilaya ya Nyamagana. Wilaya hii ipo kati ya Latitudo, $2^{\circ}15'$ na $2^{\circ}31'$ Kusini mwa mstari wa Ilkweta, na ipo kati ya Longitudo $32^{\circ} 45'$ na 33° Mashariki. Wilaya ya Ilemela ni kati ya Wilaya saba za Mkoa wa Mwanza. Wilaya zingine ni pamoja na Ukerewe, Magu, Nyamagana, Misungwi, Kwimba na Sengerema.

1.4 IDADI YA WATU

Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, wilaya ya Ilemela ina jumla ya watu 343,001 wanaume wakiwa 164,718 na wanawake 178,283 kati ya jumla ya watu 2,772,509 wa mkoa wa Mwanza ambapo ni sawa na 12% ya wakazi wote wa Mkoa wa Mwanza. Aidha, kwa makadirio ya mwaka 2020 wilaya inakadiriwa kuwa na jumla ya watu 472,807 ambapo wanaume ni 228,504 na wanawake ni 244,303.

1.5 UTAWALA

Wilaya ya Ilemela ina Tarafa 1, Kata 19 na Mitaa 171. Kwa upande wa majimbo ya uchaguzi, Wilaya pia imejumuisha jimbo la uchaguzi la Ilemela ambalo Mbunge wake anatoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula. Aidha, Wilaya kimaendeleo inahudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ambayo ina jumla ya Waheshimiwa Madiwani 26 ambao mionganini mwao Madiwani wa kuchaguliwa ni 19 na wa kuteuliwa ni 7. Wilaya ina jumla ya watumishi wa umma 3,305 wakiwemo wanaume 1,327 na wanawake 1,978.

1.6 HALI YA HEWA

Wilaya ya Ilemela hupata mvua kati ya mm 700 na mm 1000 kwa mwaka; katika misimu miwili kati ya miezi ya Oktoba na Disemba kila mwaka na kati ya mwezi Februari na Mei kila mwaka. Kiwango cha joto ni kati ya nyuzi joto za centrigrade 25.7 na nyuzi za centrigrade 30.2 majira (miezi) ya joto na nyuzi joto 15.4 na 18.6 kwa majira (miezi) ya baridi.

1.7 SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Wakazi wengi katika Wilaya wanajishughulisha na shughuli za kiuchumi katika sekta binafsi ambayo imechukua nafasi kubwa katika kutoa ajira na kujipatia kipato. Katika Sekta hii shughuli za kiuchumi ambazo wananchi wanajishughulisha ni pamoja na uvuvi, biashara za bidhaa mbalimbali, uendeshaji wa viwanda vya uzalishaji na usindikaji, kilimo hasa kwenye kata za pembezoni ambako bado kuna maeneo ya kilimo, ufugaji wa mifugo mbalimbali na wengi wao wanatumia ufugaji wa ndani. Aidha, wananchi wengi wameajiriwa katika makampuni binafsi ambayo yanatoa huduma za aina mbalimbali katika wilaya.

2.1 SEKTA YA ELIMU MSINGI

Wilaya ina jumla ya shule za Msingi 130, kati ya hizo 76 ni za Serikali na 54 ni za binafsi. Kuna jumla ya wanafunzi 80,869 kati yao wavulana ni 39,309 na wasichana ni 41,560. Kutokana na serikali kutoa elimu bila malipo na kuboresha miundombinu ya kujifunza na kujifunzia, uandikishaji wa watoto wa darasa la awali umepanda kutoka watoto 7,081 mwaka 2021 hadi watoto 7,200 mwaka 2022. Pia, uandikishaji wa darasa la kwanza umepanda kutoka wanafunzi 11,482 mwaka 2021 hadi wanafunzi 12,485 mwaka 2022.

2.2 SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

Wilaya ya Ilemela ina jumla ya shule za Sekondari 54 kati ya hizo shule 32 ni za Serikali na shule 22 ni za binafsi. Kuna jumla ya wanafunzi 33,168 wamesajiliwa katika Shule za Sekondari wakiwemo wasichana 17,349 na wavulana 15,819. Kutokana na serikali kutoa elimu bila malipo na kuboresha miundombinu ya kujifunza na kujifunzia, udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022 ni 10,502 sawa na asilimia 102 ya matarajio. Pia, serikali imeboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia katika shule zenyenye masomo ya kidato cha tano na cha sita.

2.3 SEKTA YA MAJI

Mamlaka ya Maji Safi na Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA) inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Ilemela kwa kuzingatia Sera ya Maji ili kufikia lengo la asilimia 95% ya kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama ifikapo mwaka 2025. Hadi sasa kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama katika Wilaya ni asilimia 90% na kiwango hiki kinatarajiwa kupanda mara baada ya miradi inayoendelea na utekelezaji kukamilika.

2.4 SEKTA YA BARABARA.

Wilaya ya Ilemela ina mtandao wa barabara wenye jumla ya Kilomita 875.8, kati ya hizo Kilomita 35.26 ni barabara za lami, Kilomita 2.07 ni barabara za mawe, Kilomita 1.52 ni barabara za zege, Kilomita 60.18 ni barabara za changarawe na Kilomita 776.83 ni barabara za udongo. Barabara hizi zimekuwa zikhudumiwa na fedha za kutoka Serikali Kuu pamoja na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 Wilaya imepokea kiasi cha Tsh. 2,730,191,455.68 ambazo zimetumika katika ujenzi wa makalavati, mitaro na madaraja, kuchonga na kujenga barabara na kuzibua mitaro.

2.5 SEKTA YA AFYA

Wilaya ya Ilemela ina jumla ya vituo 64 vya kutolea huduma za afya ambapo vya Serikali ni 23, Taasisi binafsi ni 4, Mashirika ya Dini 3 na watu binafsi 34. Huduma zinazotolewa katika vituo hivi ni huduma za wagonjwa wa nje (OPD), uzazi na watoto, ushauri nasaha, kupima na kutoa huduma za afya shulenii. Wilaya inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya hospitali ya Wilaya ili kuboresha huduma ambapo jumla ya Tsh. 3,100,000,000.00 zimetolewa na Serikali Kuu kwa

ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Hospitali mpya ya Wilaya katika juhudini za kuimarisha sekta ya afya kwa wananchi.

2.6 SEKTA YA MAZINGIRA

Wilaya ya Ilemela imeendelea na zoezi la usafishaji mji kupitia vituo 16 vya kukusanya taka ngumu katika kata mbalimbali. Wilaya imeingia mikataba ya uzoaji wa taka ngumu na Mawakala ambapo wastani wa tani 42,967.89 huzolewa na kupelekwa Dampo kwa mwaka. Aidha, ili kuimarisha usafi wa mji, tunaendelea kuwashirikisha Wadau, Wananchi, Taasisi za Umma na binafsi kushiriki katika zoezi la usafi na kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzolea taka.

2.7 SEKTA YA KILIMO

Eneo linalofaa kwa kilimo katika Wilaya ya Ilemela ni hekta 11,074. Hadi sasa eneo linalolimwa ni hekta 5,369 sawa na 48% ya eneo lote. Hata hivyo kutokana na kukua kwa mji na maeneo ya makazi, eneo la kilimo limeendelea kupungua huku wakulima wengi wakihamishia shughuli zao za kilimo Wilaya jirani za Magu, Misungwi na Busega. Mazao yanayolimwa ni pamoja na mpunga, mahindi, mihogo, mtama, maharage, kunde na mazao ya bustani. Wakulima wengi wanapata kipato chao kutokana na kilimo cha bustani ambacho kinachukua karibu hekta 37.

2.8 SEKTA YA USHIRIKA

Katika sekta ya Ushirika kazi kubwa inayofanya na sekta ya ushirika ni kuhamasisha jamii kuanzisha vyama vya ushirika michepwo yote, kutoa elimu kwa wanaushirika na jamii kwa ujumla kuhusu masuala ya ushirika, kufanya ukaguzi kupima ufanisi wa shughuli zinazofanya na vyama vya ushirika na kufufua, kusimamia na kuendeleza vyama vya ushirika. Halmashauri ina vyama vya ushirika 26 vyenye jumla ya wanachama 3,983 wanaume 2,097 na wanawake 1,872 na Vikundi/Taasisi 14. Vyama hivi vina mtaji wa TZS 2,663,064,549.00 unaotokana na hisa, akiba na amana na vimefanikiwa kutoa kiasi cha mikopo ya Tsh. 30,337,054,390.87. Shughuli kuu zinazofanywa na vyama hivi ni kuweka akiba na kukopesha wanachama kwa masharti nafuu na riba ndogo, kulima na kuuza mazao ya mchanganyiko, kununua na kuuza samaki na mazao yake ndani na nje ya nchi pamoja na kusindika maziwa.

2.9 SEKTA YA MIFUGO

Wilaya ya Ilemela wafugaji hujishughulisha na ufugaji wa ndani kwenye kata zilizopo maeneo ya mjini. Wilaya ina jumla ya Ng'ombe 7,148 wa asili na kisasa, Mbuzi 3,977, Kondoo 653, Punda 75, Nguruwe 7,634, Kuku 8,654 na Mbwa 919. Aidha, Wilaya kwa kushirikiana na Taasisi binafsi hutoa huduma za ugani katika kuwaelimisha wananchi kuachana na ufugaji usio na tija na kufuga kisasa, kutoa huduma za chanjo dhidi ya magonjwa hatarishi kwa mifugo na afya ya jamii, kuhamilisha ng'ombe na kutoa elimu ya uanzishwaji wa mashamba darasa ya malisho na kuwashauri wafugaji kujiunga katika vikundi ili waweze kusajiliwa na kukopesheka.

2.10 SEKTA YA UVUVI

Wilaya ya Ilemela wananchi wake wengi wanajishughulisha na uvuvi ambapo Wilaya ina jumla ya mialo 15 na kati ya hiyo mialo 3 ni mialo teule ambayo hupokea na kusafirisha samaki kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Wilaya ina Soko moja la kimataifa la samaki (Mwaloni Kirumba), Viwanda 3 vya kuchakata minofu ya samaki, na viwanda vidogovidogo 12 vya kugandisha na kuchakata mazao ya samaki. Sekta ya Uvuvi inatoa mchango mkubwa katika uchumi wa Wilaya na Taifa kwa kuwapatia wananchi ajira, lishe bora na kipato.

2.11 SEKTA YA MAPATO

Wilaya ya Ilemela imefanikiwa kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mifumo ya TEHAMA ambapo mapato yameongezeka kutoka Tsh. 8,591,229,900.00 Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi Tsh. 10,123,776,753.35 Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato, Wilaya inatumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyote na hatua hii imesaidia kudhibiti upotevu wa mapato. Wilaya kwa mwaka 2021/2022 imefanikiwa kuboresha masoko 7 ambayo yametanua wigo wa biashara kwa wananchi. Jumla ya biashara 5835 zimesajiliwa kwenye mfumo na kupewa leseni. Aidha, Ujenzi wa stendi mpya ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo umekamilika na ni matarajio ya Wilaya kuongeza kiwango cha mapato kutokana na makusanyo ya mradi huo hatua ambayo itapandisha mapato ya ndani kutoka Tsh. 10,123,776,753.35 hadi Tsh. 13,524,000,000.00 kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023.

2.12 SEKTA YA ARDHI

Wilaya ya Ilemela imefanikiwa kuongezeka kwa maeneo ya ardhi yaliyopangwa kimipangomiji ambapo hatua hii imetokana na juhudzi za Mheshimiwa Mbunge Dkt. Angeline Mabula kusaidia upatikanaji wa fedha za kulipa fidia maeneo ya miradi ya upimaji wa viwanja pamoja na kulipa fidia za wananchi waliopisha maeneo ya taasisi. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imetenga fedha kiasi cha Tshs. 1,000,000,000.00 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa miundombinu ya barabara zitakazoteklezwa kwa mpango wa TACTIC kupitia Benki ya Dunia pamoja na fidia kwa wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya taasisi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2021/2022 Halmashauri imelipa wananchi fidia jumla ya Tsh. 8,110,934,703.64

2.13 SEKTA YA NISHATI

Wilaya ya Ilemela inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme “PERI URBAN ELECTRIFICATION” ambapo hatua ya usanifu inaendelea. Mradi huu unatekelezwa katika kata 8 za Bugogwa, Shibula, Kayenze, Kiseke, Nyamhongolo, Buswelu, Kahama na Sangabuye. Mitaa 38 ya Kihiri, Shibula, Ibaya, Ilalila, Bulyanhulu, Kasamwa, Igombe B, Kisundi, Iseni, Isenga, Nsumba, Zenze, Nyamadoke, Iwelyashinga, Ibinza, Ikigijo, Bubumla, Mtakuja, Ilamba, Kagihwa, Bujingwa, Buhyila, Lukobe, Buteja, Isela, Magaka, Wihunya, Kadinda, Sangabuye, Isensa, Nyafula, Nyamiswi, Ilekako, Mg’wang’wila, Ihalalo, Imalang’ombe, Lwashi na Igumamoyo. Mradi huu unatarajiwa kuhudumia wateja zaidi ya 6,392.

3. HALI YA ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama katika wilaya ya Ilemela ni shwari pamoja na kuwa yapo matukio madogo madogo ambayo yanashughulikiwa na vyombo vyetu vya dola. Wilaya inaendelea kuhimiza ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama kwa kila mwananchi kutambua kuwa suala la ulinzi na usalama ni jukumu lake na anao wajibu wa kushirikiana na vyombo vya Dola kwa kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu na uvunjaji wa amani. Kwa ujumla, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inaendelea kushirikiana na vyombo vya Usalama, Taasisi, Mashirika binafsi na wananchi kwa pamoja katika kuimarisha usalama wa Wilaya yetu.

4. FURSA ZILIZOPO

Wilaya ya Ilemela ina fursa ambazo zikitumiwa ipasavyo uchumi unaweza kukua kwa kiwango kikubwa na kuchangia zaidi pato la Taifa. Zifuatazo ni baadhi ya fursa nyingi zilizopo katika Wilaya; uwepo wa Ziwa Victoria, uwepo wa Uwanja wa Ndege, Uwepo wa vyo vyua ufundi na Jiografia nzuri ya mkoa wa Mwanza kama kitovu cha uchumi kwenye ukanda wa maziwa makuu na Ardhi.

5. CHANGAMOTO

Mheshimiwa Rais, Wilaya ya Ilemela inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli zake za kuwaletea maendeleo wananchi. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zilizopo; Mtandao mdogo wa barabara za lami, baadhi ya kata kuwa na mawasiliano hafifu ya mitandao ya simu, ukosefu wa maji na umeme kwenye baadhi ya kata na upungufu wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

6. MPANGO WA MWELEKEO WA WILAYA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO KUANZIA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 – 2025/2026

6.1 UTAWALA BORA

Katika kuzingatia misingi ya Utawala Bora kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla, Halmashauri itazingatia yafuatayo:-

- Kujenga jamii yenyeye ari na uhuru wa kujieleza, kuishi mahali popote nchini, kushiriki katika masuala ya kisiasa kwa kuzingatia maadili na sheria za nchi.
- Kusimamia nidhamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji miongoni mwa viongozi, watumishi wa umma na wafanyakazi wengine.
- Kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, usawa na haki.
- Kuongeza idadi ya watumishi kwa kusimamia ajira mpya.
- Kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa wakati, kwa haki na uadilifu.
- Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wa Halmashauri kutoa huduma kwa wananchi kutoka kiwango cha Tsh. 10,123,776,753.35 mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kiwango cha Tsh. 20,286,172,529.00 ifikapo mwaka wa fedha 2025/2026.

- Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato.
- Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ubora kulingana na thamani ya fedha iliyotumika (value for money).

Vile vile, katika eneo la utawala bora, Halmashauri itahakikisha inasimamia utekelezaji wa Ahadi za Mheshimiwa Rais, alizotoa kwa upande wa Wilaya ya Illemela zinatekelezwa ifikapo mwaka 2025. Ahadi hizo ni zifuatazo:-

- Kuongeza miundo mbinu ya vyoo mashulenii.
- Kuongeza na kuboresha miundombinu ya madarasa.
- Kutengeneza na kukarabati miundo mbinu ya barabara.
- Kuboresha huduma za afya.
- Kuongeza upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya.
- Kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na wale mavu.
- Kupeleka umeme katika mitaa 56 iliyobaki kati ya Mitaa 171.

6.2 SEKTA YA MIUNDOMBINU

Katika kuhakikisha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi inaboreshwia ifikapo 2025, Halmashauri kwa kushirikia na TARURA itatekeleza yafuatayo:-

- Kuongeza mtandao wa barabara kutoka 70% mwaka 2020 hadi 80% mwaka 2025.
- Kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka 65% mwaka 2020 hadi 75% mwaka 2025.
- Kuongeza urefu wa barabara za mijini na vijiji zilizojengwa kwa kiwango cha lami kutoka 10% mwaka 2020 hadi 25% mwaka 2025 ambapo mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Buswelu-Busenga-Cocacola, Mbogamboga- Nyamadoke-Nyamhongolo, Kahama-Shibula-Tx, Airport- Igombe-Kayenze, Ilaila-Kabusungu-Sangabuye na Pasiansi-Lumala-Kiseke inaendelea na utekelezaji wa awali.
- Kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea kujengwa ambayo ni mradi wa stendi ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo.
- Kusimamia utekelezaji wa miradi mipya itakayotekelze na Serikali kwa ushirikiano na Benki ya Dunia ambayo ni soko Kuu la Kisasa Kirumba, barabara za kiwango cha lami za Buswelu-Busenga-Cocacola na

Mbogamboga-Nyamadoke-Nyamhongolo pamoja na mradi wa ujenzi wa mifereji mikubwa ya kutiririsha maji katika mto Kirumba na Mirongo.

6.3 SEKTA YA ELIMU

Katika kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza mambo yafuatayo:-

- Kujenga vyumba vya madarasa 300, maabara za sayansi 17, matundu ya vyoo 1000, madawati 12,000 na nyumba za Walimu 10 ambapo kwa sasa kuna madarasa 1006, maabara za sayansi 69, matundu ya vyoo 1234 na nyumba za walimu 178 hatimaye kuanzisha shule mpya 5 za msingi na 5 za sekondari.
- Kuimarisha miundombinu ya shule za sekondari Sangabuye, Buswelu na Kayenze kwa ajili ya kidato cha tano na sita.
- Kushirikiana na sekta binafsi, asasi za kiraia zikiwemo taasisi za dini na kutoa fursa za upatikanaji wa elimu.
- Kuimarisha misingi ya elimu ya kujitegemea, kuanzisha elimu ya kujitegemea (EK) ya bustani za mbogamboga na kilimo cha mazao ya chakula kwa shule zenyenye maeneo.
- Kuendeleza mpango wa kutoa Elimu Bila Malipo kwa shule za msingi na sekondari.
- Kuhakikisha kuwa shule za msingi zinatoa elimu ya awali kwa ufanisi kwa kuweza kuboresha miundombinu iliyopo.
- Kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi yakiwemo Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia na kuongeza upatikanaji wa walimu wakufundisha masomo hayo.
- Kuimarisha shule 2 za michepuo Kilimo na Biashara kwa kuzipatia vifaa vya kisasa.
- Kuajiri walimu zaidi wa masomo ya sayansi ili kuongeza nafasi za wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi na Hisabati hususan watoto wa kike.

6.4 SEKTA YA AFYA

Katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya na siha bora ifikapo 2025, Halmashauri itasimamia yafuatayo:-

- Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto na kuzitoa bila malipo ili kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.
- Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi katika vituo vyote vya kutolea huduma ya afya.
- Kuhamasisha jamii umuhimu wa matumizi ya vyandarua 600,000 vilivyowekwa dawa na upuliziaji wa viatilifu ukoko katika kuta za nyumba.
- Kutoa elimu ya kupambana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukizwa
- Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya.
- Kujenga zahanati mpya 4 katika mitaa ya Nyamadoke, Masemele, Lumala na Bezi, kujenga vituo vipyta vya afya 3 katika kata za Buswelu, Kayenze na Kiseke pamoja na kujenga Chuo cha Afya katika eneo la hospitali ya wilaya.
- Kupunguza idadi ya watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu na ukondefu kwa kuhimiza kilimo cha mbogamboga ili kupata lishe bora.
- Kuwajengea uwezo wataalam wa afya ili watoe huduma za afya na lishe kikamilifu.
- Kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi na unyanyapaa hatimaye kuongeza nguvu kazi katika uzalishaji mali.
- Kuimarisha kamati za kuthibiti UKIMWI na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa huduma za UKIMWI ili kubaini changamoto.
- Kuimarisha huduma za matibabu bila malipo kwa wazee, kuimarisha huduma za msingi kwa wazee na kuimarisha mabaraza ya wazee katika Kata 19 pamoja na mabaraza ya vijiji.
- Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na matibabu ya bima ya afya kupitia mpango wa iCHF hadi kufikia wanachama 45,000 ifikapo mwaka 2025 kutoka idadi ya wanachama 10,327 mwaka 2020.
- Kuboresha rejista ya watu wenye ulemavu itakayotoa taarifa sahihi, kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwawezesha kiuchumi watu wenye ulemavu na kujenga miundombinu rafiki ili kuhakikisha watu wenye ulemavu waweze kufikia huduma kirahisi.

6.5 SEKTA YA ARDHI

Katika kuendeleza rasilimali ardhi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha kupanga na kupima ardhi yote ya Manispaa ya Ilemela kwa kuzingatia mpango kabambe wa Jiji la Mwanza wa mwaka 2015 – 2035.
- Kuendelea kuhifadhi taarifa za wananchi katika mfumo wa kierektroniki ili kurahisha mawasiliano baina ya Halmashauri na wamiliki wa ardhi kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ardhi na kuongeza kiwango cha mapato kutoka 5,100,000,000.00 mwaka 2021 hadi 9,225,806,451.60 mwaka 2025.
- Kurasimisha ardhi inayomilikiwa kimila na makazi yasiyo rasmi mijini ili kuwawezesha wamiliki wa ardhi kunufaika.
- Kumilikisha na kusajili vipande vya ardhi vipatavyo 500,000 na kutoa Hati miliki 520,000 ifikapo mwaka 2025.
- Kulinda na kuyaendeleza maeneo ya Ihalalo na Nyamhongolo kwa ajili ya uwekezaji kulingana na Mpango kabambe wa Jiji la Mwanza.
- Kupima maeneo yote ya fukwe za ziwa viktoria ili kuyalinda kwa ajili ya uwekezaji wa miundombinu ya utalii

6.6 SEKTA YA MALIASILI NA MAZINGIRA

Katika kuimarisha usimamizi na uhifadhi maliasili ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:-

- Kutengeneza mizinga 500 na kuigawa kwa vikundi 4 vya wafugaji nyuki maeneo ya Sangabuye na Bugongwa.
- Kuendeleza program ya upandaji miti kutoka hekta 1,500 hadi 2,000 mwaka 2025.
- Kulinda na kuimarisha fukwe za ziwa viktoria ili zisitumike holela kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika utalii.

6.7 SEKTA YA MAJI

Katika kuhakikisha huduma ya maji inawafikia zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa vijijini na zaidi asilimia 95 kwa mijini ifikapo 2025, Halmashauri itasisitiza yafuatayo:-

- Kwa kushirikiana na Mamlaka ya maji na usafi wa mazingira, Halmashauri itahakikisha ukamilishaji wa miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa ili kuhakikisha kuwa mitaa yote kandokando ya miradi hiyo inapata huduma ya maji katika kata za Bugogwa, Shibula, Buswelu, Kahama na Nyamhongolo.
- Kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua katika majengo ya Serikali, asasi za umma na nyumba za watu binafsi pamoja na uchimbaji wa visima.

6.8 SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

Katika kujenga uchumi wa viwanda, Halmashauri itazingatia yafuatayo:-

- Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo ili kunufaika na Mpango wa Kusambaza Umeme Vijijini–REA na kuongeza idadi ya viwanda vidogo vidogo kutoka 298 mwaka 2021 hadi 500 mwaka 2025.
- Kutenga maeneo maalum ya viwanda vya kati na vikubwa ili kuongeza idadi kutoka 11 mwaka 2021 hadi 30 mwaka 2025
- Kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ) ambapo Halmashauri itaendeleza mpango wa utekelezaji wa eneo maalum la uwekezaji Nyamhongolo.
- Kuweka mazingira wezeshi ya biashara na kuhakikisha zinapatikana fursa nafuu za kibashara kwa kuboresha miundombinu ya biashara iliyopo na kujenga miundombinu mipya ya masoko na barabara pamoja na miundombinu ya huduma.
- Kupunguza idadi na viwango vya tozo, ada na kodi za biashara na kuweka mfumo imara wa ufuutiliaji na tathmini ambapo Halmashauri itaendelea kupitia upya viwango mbalimbali vya tozo kulingana na hali ya uchumi.
- Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo na wakati ili kuboresha biashara zao na kulipa tozo zinazotakiwa kwa wakati.

6.9 SEKTA YA MIFUGO

Katika kuzingatia ufugaji wa kisasa ifikapo 2025, Halmashauri itajikita kuboresha maeneo yafuatao:-

- Kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji na maafisa ugani kwa kushirikiana na sekta binafsi

- Kutoa chanjo kwa mifugo kwa kuzingatia mpango na ratiba ya chanjo
- Kuongeza miundombinu ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya mifugo

6.10 SEKTA YA UVUVI

Katika kuhimiza uvuvi endelevu na wenyе tija ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:-

- Kuwaelimisha wavuvi umuhimu wa matumizi ya zana bora za uvuvi na kushirikiana kupiga vita uvuvi haramu
- Kuhamasisha wavuvi kujiunga katika vikundi na vyama vy'a ushirika vy'a msingi na kuongeza idadi ya vyama vy'a ushirika wa wavuvi kutoka 5 mwaka 2021 hadi 10 mwaka 2025
- Kuhamasisha mashirika ya umma na sekta binafsi kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda vy'a kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi pamoja na kuboresha masoko ya mazao ya uvuvi yaliyopo.
- Kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa vifaa bora vy'a uvuvi, kuzuia uzalishaji na uagizaji wa zana haramu za uvuvi na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula vy'a samaki.
- Kuboresha mialo yote katika maeneo ya uvuvi Kayenze, Igombe, Mihama, Kayenze ndogo.

6.11 SEKTA YA KILIMO

Katika kuwa na kilimo chenye tija ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:-

- Kuhakikisha upatikanaji wa huduma na zana bora za kilimo cha kisasa.
- Kuwezesha wakulima kutumia mbinu za kisasa za kilimo endelevu na chenye tija.
- Kuhifadhi maeneo maalumu ya ukanda wa kijani ili kuongeza kilimo cha mbogamboga.
- Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo kwa kuongeza idadi ya masoko kutoka 6 mwaka 2021 hadi 12 mwaka 2025

6.12 SEKTA YA USHIRIKA

Katika kujenga ushirika kwa hiari ifikapo 2025. Ili kufanikisha lengo hilo, Halmashauri itafanya yafuatayo:-

- Kuhamasisha makundi maalum kijiungu na kuanzisha vyama vya ushirika kutoka vyama 25 mwaka 2021 hadi vyama 40 mwaka 2025.
- Kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOs) kwenye Ushirika wa Mazao na Masoko (AMCOS).
- Kuhimiza uanzishwaji wa vyama 15 imara vya ushirika vya msingi.

6.13 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Katika kuhakikisha wananchi wanawekewa mazingira mazuri ili washiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza yafuatayo:-

- Kuwezesha vijana, wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri katika shughuli halali za kujipatia kipato ili kuongeza uzalishaji na kuinua uchumi wa Halmashauri.
- Kuongeza juhudzi za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kukuza kiwango cha kutoa 10% ya fedha zinazotolewa mikopo kwa vijana, wanawake na walemavu kutoka Tsh. 1,017,270,000.00 mwaka wa fedha 2021/2022 hadi Tsh. 2,286,172,529.00 ifikapo mwaka wa fedha 2025/2026
- Kuongeza utekelezaji wa miundombinu inayochochea ajira ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

6.14 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KATIKA UWEKEZAJI

Katika kujenga sekta binafsi yenye mtizamo chanya wa kuwekeza katika viwanda ifikapo 2025, Halmashauri inachukua hatua zifuatazo:-

- Kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili uwekezaji wa viwanda na kuhakikisha masuala ya mipangomiji yanatekelezwa kikamilifu kwa kufanya upimaji wa maeneo yote ya Halmashauri ifikapo mwaka 2025.
- Kupitia tena utaratibu wa utoaji vibali na kufanya maboresho, ili vibali vya ujenzi viwe vinatolewa ndani ya siku saba za kazi. Halmashauri itahakikisha shughuli za ujenzi zinafanyika kwa vibali ili kuzuia ujenzi holela usiofuata masuala ya kimipangomiji

Hassan Elias Masala

MKUU WA WILAYA YA ILEMELA